


HALMASHAURI YA MJI WA BUNDA

TANGAZO LA ZABUNI YA KUTOA HUDUMA ZA ULINZI KWENYE MAJENGO YA HALMASHAURI YA MJI WA BUNDA

1. Halmashauri ya Mji wa Bunda inakaribisha maombi ya mtoa huduma ya ulinzi kwenye majengo ya Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2023/2024.
2. Mwombaji aoneshe uzoefu wa kazi ya kutoa huduma ya ulinzi alizowahi kufanya na Serikali akionesha anuani na mawasiliano ya sehemu alizowahi kufanya kazi hiyo.
3. Mwombaji anatakiwa kuchukua kabrasha la zabuni ya ulinzi Ofisi ya Kitengo cha Manunuzi kuanzia tarehe 10.05.2023 siku za kazi na saa za kazi hadi tarehe 31.05.2023.
4. Mwombaji anatakiwa kuwasilisha kabrasha la zabuni iliyojazwa vizuri akiambatanisha leseni hai ya biashara, cheti cha usajili wa Kampuni/cheti cha mlipa kodi, kibali cha kutoa huduma ya ulinzi toka Mamlaka husika.
5. Mwombaji anatakiwa kufunga zabuni yake vizuri na juu ya bahasha iandikwe zabuni anayo omba na maombi yote yawasilishwe Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Bunda (Kitengo cha Ugavi na Manunuzi).
6. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 31.05.2023 saa 4.00 asubuhi. Zabuni zitafunguliwa siku hiyo hadharani baada ya muda wa mwisho wa kuwasilisha Zabuni mbele ya wawakilishi wa waombaji watakao kuwa wamehudhuria siku hiyo kwenye Kikao cha ufunguzi. Waombaji wanaalikwa kwenye Kikao cha ufunguzi.
7. Maombi yote yatumwe kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi,
Halmashauri ya Mji wa Bunda,
288 Barabara ya Halmashauri,
S.L.P 219
31582, BUNDA – MARA

Limetolewa na;



Emmanuel J. Mkongo
MKURUGENZI
HALMASHAURI YA MJI
BUNDA.